


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO



## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imepokea kibali cha kutekeleza ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 yenye Kumb. Na.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapo chini.

### **1. MTENDAJI WA MTAATARAJA LA III- (NAFASI 11)**

#### **Sifa za Mwombaji**

- Awe amefaulu kidato cha Nne (IV) au Kidato cha Sita (VI)
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (Cheti) "NTA Level 5" kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali katika fani zifuatazo:-
  - Utawala
  - Sheria
  - Elimu ya Jamii
  - Usimamizi wa Fedha
  - Maendeleo ya Jamii
  - Sayansi ya Jamii

#### **Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Mtaa**

- Katibu wa kamati ya Mtaa
- Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelzwa na Halmashauri katika Mtaa
- Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa
- Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa
- Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umaskini katika Mtaa

- Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote katika Mtaa
- Kuandaa na kutunza rejestra ya wakazi wote wa Mtaa
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

### **Mshahara**

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mshahara ya Serikali, yaani TGS B kwa Mwezi.

## **2. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 3)**

### **Sifa za Mwombaji**

- Awe amefaulu kidato cha Nne (IV)
- Leseni ya Daraja E au C<sub>1</sub> ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua Mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiri wa kwanza

### **Majukumu ya kazi ya Udereva**

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- Kufanya usafi wa gari na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

### **Mshahara**

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mshahara ya Serikali, yaani TGS B kwa Mwezi.

### **3. MASHARTI KWA UJUMLA**

- Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiupungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka orobaini na tano (45)
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatishe maelezo yao binafsi (C.V)
- Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha moja ya rangi katika barua ya maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- "Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (FORM IV and FORM VI RESULT SLIPS) HAVITAKUBALIWA
- Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi watusika watachukuliwa hatua za kisheria
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **04.06.2022** saa **9:30** alasiri.

**Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:**

Mkurugenzi,  
Halmashauri ya Manispaa Morogoro,  
S.L.P 166,  
**Morogoro.**

**TANGANO HILI LIMETOLEWA NA:-**

  
**ALLY H. MACHELA**  
**MKURUGENZI WA MANISPA**  
**MOROGORO**  
**23 Mei, 2022**

- Nakala: - Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
S. L. P. 2320,  
**DODOMA**
- Toyuti ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro  
**www.morogoromc.go.tz**
- Mbao za matangazo